JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na. EB.318/467/01B/70** **30/06/2025**

# TANGAZO

YAH: **UKAMILISHAJI WA UTEKELEZAJI (IMPLEMENTATION) WA MPANGO KAZI 2024/2025, UKAMILISHAJI WA TATHMINI YA UTENDAJI KAZI (ASSESSMENT) NA UANDAAJI WA MPANGO KAZI 2025/2026 PEPMIS KWA WATUMISHI WASIO WALIMU.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara anawatangazia watumishi wote wasio walimu wanaotekeleza majukumu yao kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kuwa leo tarehe **30/06/2025** saa 00.00 Usiku ndio siku ya mwisho ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa mwaka wa fedha 2024/2025. Hivyo, kila mtumishi ahakikishe anajaza shughuli zake zote kwenye mfumo wa PEPMIS kwa **asilimia 100** kwenye kipengele cha **Complete** na wasimamizi wote wahakikishe wanaidhinisha kabla ya saa **00:00 Usiku leo tarehe 30/06/2025.**

**Pili**. Wasimamizi (Supervisors) wa vituo vya kazi wote wanatakiwa kufanya uhakiki na tathmini ya shughuli zote za watumishi walioko chini (Assessment) kuanzia **01/07/2025** hadi **10/07/2025** bila kukosa.

**Tatu,** Watumishi wote wanatakiwa kuandaa Mpango Kazi (**Planning**) katika mfumo wa e-Utendaji (PEPMIS) kuanzia **01/07/2025 – 10/07/2025 bila kukosa** kwa kuzingatia kipengele cha SMART.

**Nne**, Wasimamizi (Supervisors) wanatakiwa kuidhinisha shughuli za Mipango Kazi ya watumishi walioko chini yao kabla au ifikapo tarehe **15/07/2025** bila kukosa na wanapaswa kuzingatia kipengele cha **SMART** kabla ya kuidhinisha na kwa mtumishi ambaye hatazingatia kipengele hicho kazi zake zisikubaliwe kuidhinishwa zirejeshwe na msimamizi (Supervisors) kupitia kipengele cha (**Rollback**).

**Muhimu**: Ikumbukwe kuwa kushindwa kutekeleza maelekezo haya ya ukamilishaji wa utekelezaji wa Mpango kazi wa e-utendaji (PEPMIS) 2024/2025, ukamilishaji wa tathmini (Assessment) 2024/2025 na Upangaji wa Mpango Kazi 2025/2026 utapelekea mtumishi kukosa haki zake za msingi ikiwemo kutopandishwa cheo (Daraja), kutokwenda Likizo, kutopata mikopo ya kibenki na kutopata uhamisho n.k.

Nawatakia utekelezaji mwema.

Jenifer J. Mapembe

Kny: **MKURUGENZI MTENDAJI.**

KNY: MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA (W) NGARA

S.L.P 30, Ngara, Simu:028 2226016, Nukushi:028 2226152, Barua pepe:ded@ngaradc.go.tz, Tovuti: www.ngaradc.go.tz